Arusha, Tanzania

Tovuti: www.african-court.org

Simu: +255-272-510-510

**MUHTASARI WA AMRI (UTII)**

**KAMISHENI YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU**

**DHIDI YA**

**JAMHURI YA KENYA**

**OMBI NAMBA 006/2012**

**AMRI**

**(UTII)**

**4 DESEMBA 2025**

**UAMUZI WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU**

**Arusha, tarehe 4 Desemba 2025:** Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Mahakama) ilitoa Amri (utii) katika kesi ya *Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu dhidi ya Jamhuri ya Kenya*. Amri hiyo ilitolewa kufuatia kusikilizwa kwa kesi ya utii iliyofanyika tarehe 4 Juni 2025 ambayo ilikuwa imeandaliwa na Mahakama kwa hiari yake yenyewe lakini pia kwa ombi la Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ("Mwombaji" au "Kamisheni") ambayo ilikuwa imetuma Ombi la awali mbele ya Mahakama dhidi ya Jamhuri ya Kenya ("Taifa Lililoshtakiwa") mnamo 2012.

Katika hukumu yake kuhusu Ustahili iliyotolewa tarehe 26 Mei 2017, Mahakama iliamua kwamba Taifa Lililoshtakiwa lilikiuka Ibara za 1, 2, 8, 14, 17(2), 17(3), 21 na 22 za Mkataba. Katika Hukumu iliyofuata kuhusu Fidia ("Hukumu kuhusu Fidia"), iliyotolewa tarehe 23 Juni 2022, Mahakama iliamuru kulipwe fidia ya fedha na isiyo ya fedha kwa Mwombaji. Miongoni mwa mambo mengine, Taifa Lililoshtakiwa liliamrishwa kulipa KES 57, 850, 000 kwa hasara ya mali na KES 100,000,000 kwa hasara ya kimaadili iliyoipata jamii ya Ogiek. Pia Taifa Lililoshtakiwa liliamrishwa kushauriana na jamii ya Ogiek ili kubaini ardhi zao za jadi, kutambua mipaka na kuzitenga sehemu hizi na kuwapa hati miliki ya pamoja; kuitambua jamii ya Ogiek kama watu wa asili; kuanzisha Mfuko wa Maendeleo wa Jamii; kushiriki katika mashauriano

ya maana na jamii ya Ogiek kuhusu mambo yanayowaathiri ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa Hukumu kuhusu Fidia na kutangaza uamuzi wa Mahakama.

Mahakama pia ilikuwa imeamua, katika Hukumu yake kuhusu Fidia, kwamba itafanya kesi ya umma katika tarehe itakayobainishwa baadaye ili kutathmini utii wa maagizo yake. Kwa hivyo, kusikilizwa kwa kesi kulikopelekea kutolewa kwa Amri hii kulilenga kutathmini kama, na kwa kiasi gani, Taifa Lililoshtakiwa lilikuwa limetekeleza Hukumu ya Mahakama kuhusu Ustahili na Hukumu kuhusu Fidia na kubainisha matokeo ya kisheria ya kutoitekeleza.

Katika uamuzi wake, Mahakama ilianza kwa kushughulikia mamlaka yake ya kuendesha kesi kuhusu hali ya utekelezaji. Kuhusu hili, iliamua kwamba mamlaka yake ya kuendesha kesi kama hiyo imejikita katika Kanuni ya 81(3) ya Sheria zake, Ibara ya 30 ya Protokali na Ibara ya 1 ya Mkataba. Zaidi ya hayo, ilikumbusha kuhusu mamlaka yake ya awali katika kesi ya *Suy Bi Gohore dhidi ya Côte d'Ivoire* ili kusisitiza kwamba ufuatiliaji wake wa utii unajaliza badala ya kujitwalia jukumu la Baraza la Utendaji la AU. Kwa msingi huu, Mahakama iliamua kwamba inayo mamlaka ya kuamua kama Taifa limetii hukumu yake ndani ya muda uliowekwa na kutoa maagizo yanayofaa ili kuhakikisha kuna utii.

Kisha Mahakama ilitathmini utii wa Taifa Lililoshtakiwa kwa masharti ya Hukumu yake kuhusu Ustahili. Kwa kufanya hivyo, ilizingatia kwa makini mawasilisho ya Taifa Lililoshtakiwa kuhusu juhudi ambazo lilikuwa limefanya kushughulikia ukiukaji wa Ibara za 1 na 2, pamoja na Ibara ya 14 ya Mkataba. Mahakama pia ilizingatia mawasilisho ya Waombaji kuhusu hali ya utekelezaji ya maagizo yake.

Mahakama, huku ikitambua juhudi zilizofanywa na Taifa Lililoshtakiwa, kukiwemo kuanzishwa kwa sheria na uundaji wa vikao vya mashauriano kwa ajili ya utekelezaji wa Hukumu yake, bado ilipata kuwa hatua hizi hazikusuluhisha kikamilifu ukiukaji wa kimsingi uliotambuliwa katika Hukumu ya Ustahili. Hivyo basi, ilihitimisha kuwa utii wa Taifa Lililoshtakiwa wa Hukuhu kuhusu Ustahili ulikuwa wa sehemu tu. Kwa hivyo, Mahakama iliamuru Taifa Lililoshtakiwa kuchukua mara moja hatua zote za kisheria, kiutawala au nyingine zinazohitajika ili kutekeleza kikamilifu Hukumu kuhusu Ustahili.

Kuhusu utii wa Hukumu kuhusu Fidia, Mahakama ilianza kwa kuzungumzia utii wa amri yake ya fidia kwa kuzingatia fida ya fedha na fidia isiyo ya fedha. Mahakama ilisema kwamba Taifa Lililoshtakiwa halikuwa limebainisha hatua zozote zilizochukuliwa kulipa KES 57,850,000 na KES 100,000,000 ambazo ilikuwa imeamuru. Kwa hivyo, iliamua kwamba kulikuwepo na kutotii agizo lake na kwa hivyo iliamuru Taifa Lililoshtakiwa lifanye malipo hayo yaliyoamriwa mara moja.

Kuhusu agizo la kutambua, kuweka mipaka, kutengwa na kutoa hati miliki ambazo jamii ya Ogiek ilistahili kupata, Taifa Lililoshtakiwa liliifahamisha Mahakama kwamba Majopo Kazi yameanzishwa kusaidia katika kutambulisha, kuweka mipaka, kutenga na kutoa hati miliki za ardhi hiyo.

Baada ya kutathmini mawasilisho ya Wadaawa, Mahakama ilikubali kwamba ingawa Taifa Lililoshtakiwa lilikuwa limepiga hatua katika kutii masharti ya Hukumu yake, hatua hizi hazikuwa zinatosha. Mahakama ilisisitiza kwamba kwa mujibu wa masharti ya Hukumu yake kuhusu Fidia, lazima mchakato wa utambuaji, uwekaji mipaka, utengaji na utoaji wa hati miliki ya ardhi ya jadi ya Ogiek ufuate mchakato wazi, wa mashauriano ambao matokeo yake yatakuwa utoaji hati miliki ya pamoja kwa jamii ya Ogiek. Mahakama pia ilipata kwamba Taifa Lililoshtakiwa halikuwa limeweka njia halisi, yenye muda maalumu kwa utekelezaji wa agizo hili. Hivyo basi Mahakama iliamua kwamba agizo la utambuaji, uwekaji mipaka na utoaji wa hati miliki kwa ardhi ya jadi ya jamii ya Ogiek halikuwa limezingatiwa na ikaagiza Taifa Lililoshtakiwa kuchukua hatua zinazostahili mara moja ili kurekebisha hali hiyo.

Kisha Mahakama ilichunguza suala la ardhi ya jadi ya jamii ya Ogiek iliyo kwenye matumizi maalumu au mikataba ya kupangisha. Ilibainisha kwamba Hukumu yake kuhusu Fidia illiihitaji Taifa Lililoshtakiwa kubaini matumizi maalumu na mikataba ya kupangisha iliyopo kwenye ardhi ya jamii ya Ogiek na kuanzisha mazungumzo na mashauriano na watu wa tatu na jamii ya Ogiek, kuhusu ulipaji fidia na urejeshaji wa hali ya zamani pale ambapo makubaliano hayangepatikana. Huku ikikubali kwamba michakato ya haki ilikuwa muhimu katika kutatua suala la matumizi maalumu na mikataba ya kupangisha ardhi ya jadi ya jamii ya Ogiek, Mahakama ilipata kwamba, katika hali halisi, Taifa Lililoshtakiwa lilikuwa halijaanza kutekeleza wajibu wake na hivyo halijatii agizo hili.

Kuhusu agizo la kutambua Ogiek kama jamii ya asili, Taifa Lililoshtakiwa lilidai kwamba katika sensa yake ya kitaifa ya 2019, pamoja na sheria zake za ndani zinazotokana na desturi ya kesi zilizotangulia, tayari jamii ya Ogiek ilikuwa inatambuliwa kikamilifu. Mwombaji, kwa upande wake, alidai kwamba utambuzi kiishara bila utekelezaji halisi wa haki za ardhi na mashauriano haukuwa unatosha na alibainisha ukosefu wa ufuatiliaji kisheria au kitaasisi wenye maana tangu mwaka 2022. Mahakama ilisisitiza kuwa utambuzi kamili na wa kweli unahitaji kwamba jamii ya Ogiek itekeleze haki zake kwa misingi sawa na wengine. Ilipata kwamba hili bado halijafikiwa na ikahitimisha kwamba agizo la utambuaji halikuwa limetekelezwa kikamilifu, hivyo ikahitaji Taifa Lililoshtakiwa kuchukua hatua madhubuti zaidi ili kutii masharti ya Hukumu.

Kuhusu agizo la Mahakama la Taifa Lililoshtakiwa kuwezesha haki ya mashauriano ya jamii ya Ogiek, Taifa Lililoshtakiwa lilieleza kuwa lilikuwa limehusisha jamii ya Ogiek kwa kiasi kikubwa kupitia majopo kazi na kamati inayohusisha wizara mbalimbali, na ilitoa orodha za mahudhurio kuthibitisha dai hilo. Hata hivyo, Mwombaji alitoa ushahidi unaoonyesha kuwa maamuzi makuu, yakiwemo uondoaji wa vikwazo juu ya miamala ya ardhi na vitendo vya utekelezaji, vilizchukuliwa bila mashauriano ya kina na ya awali.

Mahakama ilisisitiza kuwa lazima mashauriano, hasa na watu wa asili, yawe yenye maana, yanayozingatia utamaduni na yanayoendelea, na lazima yaheshimu taratibu zao za kufanya maamuzi. Ilipata kwamba, ingawa kuna mashauriano yaliyokuwa yamefanyika, hayakukidhi kiwango kilichowekwa katika Hukumu kuhusu Fidia. Hivyo basi, Mahakama iliamua kwamba maagizo kuhusu mashauriano na kutorudia hayajatekelezwa kikamilifu na ikaamuru Taifa Lililoshtakiwa lichukue hatua za haraka na maalumu kutekeleza masharti ya amri yake.

Kuhusu uanzishwaji wa mfuko wa maendeleo ya jamii na kamati ya kusimamia mfuko huo, Taifa Lililoshtakiwa lilieleza kwamba mipango ya kisheria na kiuchumi ilikuwa changamano na ilihitaji muda. Hata hivyo, Mwombaji alibainisha kwamba hakukuwepo na mfuko wala kamati ya kuusimamia, na kwamba hakukuwa na ushahidi wa hatua madhubuti kuhusu uanzishaji wake zilizochukuliwa. Mahakama iliamua kwamba hakukuwa na ushahidi wa maendeleo halisi na ikaagiza Taifa Lililoshtakiwa lianzishe mara moja mfuko huo na kuhakikisha kuwa kamati simamizi inaanza kufanya kazi.

Kuhusu utangazaji wa hukumu, Taifa Lililoshtakiwa lilitaja mabadiliko ya kisiasa kama sababu ya kushindwa kwake kuitangaza hukumu na muhtasari kama ilivyoagizwa; Mahakama ilibaini kwamba Taifa Lililoshtakiwa lilikuwa bado halijatimiza wajibu wake wa kutangaza maamuzi hayo na ikakataa mabadiliko ya kisiasa kama sababu halali ya kueleza kwa nini tangazo lilikuwa halijatolewa bado. Kwa hivyo iliamrisha Taifa Lililoshtakiwa kutangaza mara moja Hukumu kuhusu Ustahili pamoja na Hukumu kuhusu Fidia, pamoja na mihutasari yake, kama ilivyoagizwa katika aya ya xiv ya Hukumu kuhusu Fidia.

Kuhusu utoaji wa ripoti, Mahakama ilisema kwamba kulingana na masharti ya Hukumu yake kuhusu Fidia, ripoti ya utekelezaji, kutoka kwa Taifa Lililoshtakiwa, ilikuwa inatakiwa kuwasilishwa katika muda wa miezi kumi na miwili baada ya kufahamishwa (kufikia Juni 2023) lakini iliwasilishwa Mei 2025, karibu miaka miwili baadaye. Huku ikikiri kwamba ripoti ilikuwa imetolewa ambayo ilikuwa na maelezo kuhusu hatua zinazochukuliwa ili kutimiza uamuzi wa Mahakama pamoja na changamoto zinazokabiliwa na Taifa Lililoshtakiwa, bado Mahakama ilishikilia kwamba amri yake kuhusu uwasilishaji wa ripoti ya utekelezaji haikuwa imezingatiwa ndani ya muda uliowekwa.

Kisha Mahakama ilishughulikia madai ya Mwombaji ya ukiukaji unaoendelea na ombi la hatua za muda. Mwombaji alidai kuwepo kwa ukiukaji unaoendelea, ikiwa ni pamoja na kufukuzwa kutoka kwenye ardhi hiyo na kuharibiwa kwa nyumba na mali za jamii ya Ogiek. Taifa Lililoshtakiwa lilieleza kwamba lilikuwa linatekeleza mabadiliko katika mazingira changamano ya kijamii na kisiasa. Mahakama ilikubali uzito wa madai ya Mwombaji lakini ikashikilia kwamba haja ya hatua za muda ilikuwa inatokana moja kwa moja na kushindwa kwa Taifa Lililoshtakiwa kutekeleza maamuzi ya Mahakama. Kwa hivyo, ilikataa kutoa hatua za muda za ziada, ikizingatia kwamba utii mkamilifu wa maamuzi yake ungeshughulikia madhara yaliyodaiwa na Mwombaji.

Kuhusu gharama, Mahakama iliamuru kwamba kila mdaawa alipe gharama zake mwenyewe.

Taarifa zaidi kuhusu kesi hii, ikiwa ni pamoja na matini kamili ya hukumu ya Mahakama ya Afrika, inaweza kupatikana kwenye tovuti katika: https://www.african-court.org/cpmt/details-case/0062012

Kwa maswali mengine yoyote, tafadhali wasiliana na Masijala kwa barua pepe registrar@african-court.org

*Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ni mahakama ya bara iliyoanzishwa na Mataifa Wanachama wa Umoja wa Afrika ili kuhakikisha kuna ulinzi wa haki za binadamu na watu barani Afrika. Mahakama ina mamlaka juu ya kesi na migogoro yote iliyowasilishwa kwake kuhusu ufasiri wa matumizi ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu na hati zingine zozote zinazofaa za haki za binadamu zilizoidhinishwa na Mataifa yanayohusika. Kwa habari zaidi, tafadhali tembelea tovuti yetu katika www.african-court.org.*